UFUNGUZI WA MAFUNZO KWA WADADISI NA WASIMAMIZI WA UTAFITI WA MASUALA YA JINSIA, MILA, DESTURI, SHERIA NA TAMADUNI TANZANIA (SIGI) MWAKA 2020 ULIOFANYIKA MJINI BABATI MKOANI MANYARA TAREHE 2-12-2020

Afisa Tawala wa Mkoa wa Manyanyara ndugu Missaile R. Mussa akitoa hotuba kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mheshimiwa Joseph Mkirikiti katika uzinduzi wa mafunzo ya Wadadisi na Wasimamizi wa Utafiti wa Masuala ya Jinsia, Mila, Desturi, Sheria na Tamaduni Tanzania 2020 yaliyofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Mkoani Manyara tarehe 2/12/2020

Afisa Tawala wa Mkoa wa Manyara kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara alianza kwa kueleza madhumuni ya utafiti huo ambayo ni kutoa ushahidi na kuelewa dhana ya ubaguzi katika ngazi za Kitaifa na Kimkoa ikiwa ni pamoja na kuunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania katika kutatua changamoto za kisera zinazohusiana na kutokuwepo na usawa wa kijinsia.

Hata hivyo aliwaeleza washiriki wa mafunzo hayo kuwa utafiti huo unalenga kuhakikisha kuwa takwimu za masuala ya jinsia yanayohusiana na mila, desturi, sheria na tamaduni zinapatikana ili ziweze kutumika katika kuhuisha na utungaji wa sera na kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji kwa wanawake.

Alielezea pia kuwa Takwimu zitakazopatikana katika utafiti huu zitatumika katika kupanga mipango ya maendeleo ili kuboresha haki na hali za wanawake na wasichana wa Tanzania na kuleta usawa wa jinsia kwa kuondoa ubaguzi katika jamii na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo nchini.

Aidha, aliongeza kuwa Utafiti huo wa Masuala ya Jinsia, Mila, Desturi, Sheria na Tamaduni Tanzania 2020 ni moja ya utafiti wenye lengo la kusaidia kutathmini na kufuatilia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030 hususan lengo la 5 linalohusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kwa upatikanaji takwimu za jinsia.

Afisa Tawala kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa aliwataka washiriki wa Utafiti huo ambao unafanyika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania kutekeleza majukumu yao ya kukusanya taarifa na kuhakikisha wanazingatia nidhamu ikiwemo kuvaa mavazi nadhifu ambayo sio tu yanayolingana na utamaduni wa Mtanzania lakini pia yawe kwa mujibu wa maadili ya utumushi wa umma.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Takwimu za Kijamii Ndugu Ruth Minja akitoa hotuba kwa niaba ya Mtakwimu Mkuu Dkt. Albina Chuwa katika ufunguzi wa mafunzo ya utafiti wa SIGI huko Babati Mkoani Manyara.

Ndugu **Ruth Minja Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Takwimu za Kijamii** alisoma hotuba kwa niaba ya Mtakwimu Mkuu Dkt. Albina Chuwa na alielezea kuwa Utafiti huu utafanyika katika maeneo ya kuhesabia watu 217 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo kwa **Tanzania Bara** maeneo 182 yatafanyiwa na Zanzibar maeneo 35.

Aidha, alifafanua kuwa Utafiti huu unatarajiwa kufanyika katika kaya 4,340 nchi nzima na kaya hizo zitachaguliwa kisayansi ili kupata sampuli wakilishi. Utafiti huu utawashirikisha wanakaya 8,680 wakiwemo wanawake 4,340 na wanaume 4,340.

Aidha, matokeo ya Utafiti huo yatachochea kasi ya maendeleo endelevu nchini, kiasi ambacho tutaweza kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo tuliyojiwekea katika ngazi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kama vile; Agenda ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu ya 2030, Agenda ya Maendeleo ya Afrika ya 2063 na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025.

Muakilishi kutoka Shirika linaloshughulikia Wanawake Tanzania Dkt. Mitra Sadananda alikielezea baadhi ya shughuli zilizofanyika katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) chini ya udhamini wa Shirika hilo.

Muwakilishi kutoka shirika linaloshughulikia wanawake (UN women) Dkt. Mitra Sadananda ambaye pia ni mtaalamu elekezi wa masuala ya jinsia alielezea kuwa shirika la Umoja la Wanawake Tanzania alieleza kuwa shirika hilo lilianza kufanya kazi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS) tokea mwaka 2018 kupitia programu inayoitwa Kumuwezesha Kila Mwanamke na Msichana Kuhesabiwa "**Making Every Women and Girls Count."**

Na alielezea kuwa baadhi ya shughuli zilizofanyika ni:-

- Kuweka mfumo wa takwimu za jinsia Tanzania Bara na Zanzibar
- Kuimarisha utaratibu wa uratibu wa masuala ya jinsia
- Kundeleza mikakati ya takwimu za jinsia itakayojumuishwa katika mpango kabambe wa uimarishaji wa Takwimu Tanzania (TSMP II) pamoja na Mpango Mkakati wa uimarishaji wa Takwimu Zanzibar (ZSDS).

- Kusaidia kupata baadhi ya viashiria vinavyotokana na Mpango wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kutoka katika utafiti wa mapato na matumizi ya kaya.

- Kufanya Utafiti wa masuala ya jinsia yanayohusiana na mila, desturi, sheria na tamaduni za Tanzania (SIGI)

Mwisho Dkt. Mitra alizishukuru ofisi zote mbili (NBS na OCGS) na timu nzima ya utafiti huu kwa kufanikisha uandaaji wa dodoso litakalotumika kukusanyia taarifa za utafiti huu. Alielezea pia kazi haikuwa rahisi kwani maandalizi yalifanyikabkupitia vikao vingi vya kujadili utafiti wa SIGI na vilifanyika kwa njia ya mitandao kutokana na janga la CORONA na hatimaye kufanya matayarisho ya uandaaji wa mafunzo haya muhimu ya wadadisi na wasimamizi wa utafiti huu ambayo yanafanyika hii leo.

Mkurugenzi wa Idara yaTakwimu za Kijamii katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar Ndg. Khadija Khamis Hamadi, akitowa neno la shukurani kwa Mgeni Rasmin katika hafla ya Uzinduzi wa Utafiti Babati Mkoani Manyara

Nae Muakilishi kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar Ndugu Khadija Khamis Hamad ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Takwimu za Kijamii alitowa neno la shukurani kwa mgeni rasmi kwa kukubali kuja na kutufungulia mafunzo haya ya wadadisi na wasimamizi wa utafiti wa masuala ya jinsia, mila, desturi, sheria na tamaduni za Tanzania na kutoa hotuba iliyo nzuri yenye mafunzo na nasaha ndani yake.

Pia aliahidi hotuba yake itafanyiwa kazi kuanzia ngazi ya wakufunzi, wasimamizi, wadhibiti wa ubora wa viwango mpaka ngazi ya wadadisi ambapo alisisitiza sana nidhamu wakati wa ukusanyaji wa taarifa..

Pichani Mgeni Rasmin Mhe.Joseph Mkirikita(wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Wadadisi na Wasimamizi wa Utafiti wa Masuala ya Jinsia,Mila,Destuti, Sheria na Tamaduni Tanzania (SIGI)